

**MOMBASA COUNTY ASSEMBLY****HANSARD REPORT**Wednesday, 5<sup>th</sup> October, 2016

The House met at 9.22am.

*(The Deputy Speaker (Hon. Mswabah Rashid) in the Chair)***PRAYERS****The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Members you may sit, yes Clerk.**PAPER**

Hon. Amir Thoya.

**Hon. Thoya:** Thank you Mr. Speaker sir, with your permission and the permission of this Hon. House I wish to table a Report on the dangerous open drain at Mwangosi Village, Airport Ward.

But as it was necessitated by the Statement by Nominated Member of the County Assembly Hon. Mary Akinyi. I wish to table...

*(Paper laid)***The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank you very much, the procedure is you table the Report then it comes as a Notice of Motion then as a Motion at a later date.

So Hon. Amir Thoya, this Report will go before the House Business Committee and it will be allotted a day then it will come as a Motion, thank you, yes Clerk.

**MOTION**

Hon. Zeinab Kithinzi.

**Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi:** Thank you Hon. Speaker. Mr. Speaker Sir I beg to move the following Motion.*(Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi read Motion)**"THAT AWARE that the County Assembly annually incurs tremendous expenditure on transport and travelling expenses for Members and staff.**FURTHER AWARE that Members and staff of the County Assembly travel frequently officially within and outside the County in discharge of their duties and responsibilities.**CONCERNED that these expenses could be significantly reduced if the County Assembly had welfare buses for transport and travel.**I therefore urge the County Assembly to RESOLVE that;**The County Assembly Service Board to plan, budget and purchase welfare buses for official travel and transport of Members and staff of the County Assembly in order to minimize expenditure on the same and for prudent use of financial resources".*

*(Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi ended reading the Motion)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Amir Thoya.

**Hon. Thoya:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono hoja alioleta Mheshimiwa Zeinab.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Members I will propose a question, it has been proposed that this County Assembly purchase a welfare bus for the County Assembly.

*(Question put and agreed to)*

Yes Hon. Kithinzi.

**Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kama tunavyoelewa uchumi wetu sio mzuri sana na nimeona kuna haja Bunge la Kaunti ya Mombasa iweze kununua basi ya kuwezesha na kurahisisha kazi ya hii ya Bunge letu, Mheshimiwa Spika...

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes.

**Hon. (Ms.) Akinyi:** Ahsante sana, nimesimama kumjulisha kuwa anafahamisha Nyumba hii kuwa kama uchumi wetu ni mmbaya saa hizi gari tutanunua?

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Mary you are contributing to a Motion, it's not a correction that is debating, Yes Hon. Kithinzi.

**Hon. (Ms.) Kithinzi:** Mheshimiwa Spika nafikiria sio makosa yake, kama nilivyoelezea iwapo Bunge la Kaunti ya Mombasa tutaweza kununua basi itarahisisha mambo mengi kwa sababu kuna mambo fulani ambayo hayatembeji kwa sababu hakuna usafiri.

Ningeomba hii Bunge la Kaunti yetu iweze kuniunga mkono nataka tupitishie huu mswada ili tuweze kukata gharama zengine na usafiri ukawa ni rahisi ya sisi na wafanyi kazi wetu. Ahsante mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Chairman.

**Hon. Mohamed Hatimy:** Ahsante Mr. Speaker, I request the mover of this Motion to amend the title, buses to be bus.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Mary.

**Hon. (Ms.) Akinyi:** Thank you Mr. Speaker Sir, we know very well that with amendments it has to be written.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): He is just requesting the mover of the Motion, yes Hon. Kithinzi, is it bus or buses.

**Hon. (Ms.) Zainab Kithinzi:** Mr. Speaker nafikiri ni *typing error* ilikuwa ni bus.

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Well Clerk you should note that its one bus not buses, yes Hon. Amur.

**Hon. Amur:** Mr. Speaker the Motion on the floor is a good Motion but I think the Motion the House should be told because we had budgeted for minibus for this County Assembly, how far is the issue?

*(Applause)*

Because we had budgeted I remember very well but what happened, was it purchased? was it a tender issue? Because we are going back to bring a Motion whereby it had already

been budgeted in the financial year for us to have that bus so we should be told why it was not purchased yet it was budgeted for, thank you.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Karisa Nzai.

**Hon. Nzai:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nataka kumfahamisha kwamba Mheshimiwa Kithinzi ambaye amekuwa akiongoza Mswada huu wa kununua basi iweze kupitishwa.

Mheshimiwa Spika nikipata ruhusa kutoka kwa Mwenyekiti ni kwamba tulikuwa na mipango na tayari mipango iko katika *advanced stage* ya kununua basi hilo.

Sasa sioni kwamba tunataka kulazimisha mpaka ikuwe *Motion* ya kununua basi wakati Bodi ya Bunge la Mombasa yaani *County Assembly Service Board* wako katika harakati ya kuinunua basi hii na nafikiri tatizo lilikuwa tununue basi la kutoka kwa CMC ama tununue basi kutoka kwa Kampuni zengine.

Mheshimiwa Spika Kaunti ina mipango na tulituma mmoja wetu na ndio sababu tukasema tununue basi na tayari mipango hiyo nafikiri ni siku chache tutalionga Mheshimiwa Spika ya kwamba kuna kandarasi ambayo tumetoa ya kununua basi.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa wa Mwakirunge.

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kumwambia Mheshimiwa ambaye amesimama ya kwamba sisi hatutaki kujua basi litanunuliwa CMC wala nini? Basi ni basi Mheshimiwa Spika na nafikiri toka hiyo mipango iwe kuna *financial years* zimepita nyingi.

Kwa hivyo kama anasema Bodi wananunua gari Mheshimiwa anapotosha hili Bunge na sisi tumeleta hii *Motion* ili kusukuma, nafikiria hata *site visits* tumeshindwa kwenda kwa sababu tungekuwa na basi letu *site visits* tungekua tushazienda bila shida zozote Mheshimiwa spika. Ahsante Mheshimiwa Spika.

(*Applause*)

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Karisa Nzai first we need to know whether you are supporting the Motion or you are not supporting it we need to know, are you for or against the Motion.

**Hon. Nzai:** Ahsante Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia moja...

(*Applause*)

Hata sababu ya ripoti ya basi Mheshimiwa Spika kitu kizuri huwa kinachukua muda na hatukua tunataka kufanya haraka ili tununue basi ambalo halina mpango.

Tunataka kununua basi nzuri, basi kubwa basi ambalo ndani kuna AC Waheshimiwa wakienda mahali, hata linaweza kuenda Lamu bila kuwa shida na kama unavyojua barabara ya Lamu wakati mwengine huwa iko na balaa Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Amur what is it?

**Hon. Amur:** Why is it particular in Lamu where there are so many roads in Kenya Mr. Speaker, is he targeting me or what? Protect me Mr. Speaker.

**Hon. Nzai:** Mheshimiwa Spika Lamu ndio najua wakati mwingi tukienda hua ni mbali kidogo, hatuna kinyongo wala hatuna jambo lolote tunajua Kwale bara bara safi tukitaka kuenda pande hii bara bara iko nzuri hata tukitaka kuenda Kilifi lakini tukipita kuna mahali kuelekea Lamu Mheshimiwa Spika hua kuna matatizo.

Lakini kwa sababu ya uzuri na mipango ambayo tuko nayo tununue basi nzuri, Mheshimiwa Spika naunga mkono na naamini Nyumba hii itapitisha kwa haraka na Kamati ya Fedha ambao tuko tutahakikisha tumeweza kununua basi hili kwa haraka. Mheshimiwa Spika ahsante.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Kibwana Swaleh Baya.

**Hon. Kibwana Swaleh:** Thank you Hon. Speaker, I still have an observation in this Motion because of the timing of the buying of the bus; one it did not clearly state in the Motion whether it is a 42 seater whether is it a minibus or a bus that is one.

Second Hon. Speaker we have been asking for a means of transport since we came to this Hon. House I don't know why now we are going to end our term then we are in a hurry of buying a bus.

This should be planned by the future MCAs who will be here in this House rather than we who are going for election then trying to see that we want to buy a bus we have started this for a long time, the issue of the bus we have been discussing for long for four years.

Mr. Speaker so I don't see why bring a Motion to this Hon. House that you want to purchase a bus, this is an administrative issue that is before the County Service Board who are looking for our interest.

So to me I feel the time of this Motion is not good and I think the money that should buy a bus should pay rent for our offices Hon. Speaker, we have a lot of challenges as the government we still have some more arrears for our offices.

Hon. Speaker now we are trying to divert that money for our offices for buying a bus, there are other issues of gratuity the county has not remitted our money to our accounts.

So I think our energy at this moment should be put to the things that are very important Hon. Speaker, I think I normally like to share what nominated Hon. Zainab Kithinzi said that I would be happy if now we could bring a Motion saying that the money to buy the bus should be remitted to our accounts for our gratuity then I would have supported the Motion.

But to me that the tender process that will take three months Hon. Speaker then we'll be out, next year in March there's the nomination issue which will come here and who will board that bus for site visits, nobody.

So Hon. Speaker I think as much as we are very interested we want to be comfortable travelling to Lamu to Kisumu but I think this is not the right time so let's put our energy, the resources we want to buy a bus to put to where we feel it is really important. Thank you Hon. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Amir Mohamed Thoya.

**Hon. Thoya:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono.

*(Applause)*

*Motion* iliyoletwa na Mheshimiwa Zeinab, Mheshimiwa Spika kama Bunge tuko na jukumu la kutoa muelekeo kwa jinsi mambo ya Kaunti yetu yanaweza kwenda na ni vizuri tujue ya kwamba basi hii ambayo Mheshimiwa ameomba kupitia Bunge hili liweze kununuliwa sio kwa manufaa ya wabunge pekee yake bali ni kwa moja ya manufaa ya wafanyi kazi wetu.

Na nataka tuelewe ya kwamba sisi pia ni wanasiasa na mara kwa mara wakati mwengine tunapatwa na hali ambayo inatulazimu kuweza kuchukua pengine ni watoto wa shule kutoka

sehemu moja mpaka sehemu nyengine na kama ninavyoelewa ya kwamba gharama ya basi zile ambazo ni *commercial* gharama ile iko juu na nahisi kwamba iwapo kama Bunge letu litaweza kuwa na usafiri wake itaweza pengine kupata nafasi hii mbali na kwamba inasafirisha Wabunge mbali na kwamba inasafirisha wafanyi kazi wetu ikitokea dharura kama hiyo aidha itasafirisha wanafunzi ama kwa masuala ya msiba nahisi kama inaweza kutusaidia...

*(Interruption)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Onje what is it?

**Hon. Onje:** Ahsante Mheshimiwa Spika mimi ningependa kumuuliza Mheshimiwa mwenzangu ambaye ameongea kwani hili basi ambalo tunataka kununua, tunanunulia watoto wa shule ama tunanunulia waheshimiwa...

*(Laughter and applause)*

Atufafanulie vizuri kama ni watoto shule tujue kama tunawanunulia watoto wa shule basi...

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Amir Thoya.

**Hon. Thoya:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nikijibu kwa Mheshimiwa alieulizia swali kwamba kuna neno ambalo linaitwa *welfare* pengine anahitaji *Oxford Dictionary* kuweza kutafsiriwa hiyo *welfare* inamaanisha nini?

*Welfare* inamaanisha maslahi ya kijamii ndio maana nasikitika kuona Mheshimiwa Kibwana amesema kwamba basi hili tunanunua wakati sisi tunatoka amesahau ya kwamba wafanyi kazi ambao wako hapa watabakia yeye arudi asirudi lakini basi hili litabakia...

*(Applause)*

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika cha msingi ni kuhakikisha ya kwamba basi hili linatumiwa, linaweza tumika kwa Waheshimiwa, liweze kutumika kwa wanafunzi wetu, liweze kutumika kwa wafanyi kazi wetu.

Cha msingi ni kwamba ni muhimu hoja hii ambayo imeletwa na Mheshimiwa Zeinab iweze kuungwa mkono Mwenyekiti wa Fedha yuko hapa anajua pesa tayari ishatengwa iweze kusukumwa tuweze kuhakikisha ya kwamba basi hili linapatikana watu wetu waweze kupata afueni wakati wanaposafiri. Ahsante sana Mheshimwia Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Majority Hamisi Mwidani.

**Leader of Majority Hon. Mwidani:** Mr. Speaker thank you for giving me this opportunity I also arise here to support this Motion...

*(Applause)*

Mr. Speaker I think we need to have a bus; to be very sincere sometimes we get a lot of problems when we do site visits.

Actually this is the time now we can do good things so that we can be seen we are doing them, I assure you so long as it is in the budget under docket of the Service Board we will make sure that we proceed although it has been mentioned that we have been left with a few days it doesn't matter, even whatever is here can be used by other Members when they come.....

*(Applause)*

Actually am very sure that with my hope even the drivers who are here ... *(Inaudible)*

*(Applause)*

Because Mr. Speaker am assuring this House that as the Leader of Majority in this House I will make sure that as a Board that we buy this bus. Thank you Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Hatimy.

**Hon. Mohamed Hatimy:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika kwanza nataka Nyumba hii ijue watu wameanza kubadili njia, sisi tulipewa pesa tuzipangie zile pesa tukiwa tumepatiwa mkononi, haimanishi pesa hizi tutazitumie vile tunavyotaka...

(*Applause*)

Mheshimiwa Spika pesa zimegawanya asilimia 40 ziwe ni mshahara, 30 huwa ni *Operations* na 30 huwa ni *development*.

Mheshimiwa Spika ukiangalia bajeti yenye tumepatiwa sisi ni kama tunavyojua kwamba CRA wanataka *ceiling budget* yetu sisi ni shilingi 618 milioni, 618 milioni ukitoa 418 milioni inabaki 200 milioni.

200 milioni hiyo ukitoa asilimia 30 inabaki 140 milioni, hiyo 140 milioni ukitoa asilimia 30 unabakia na kama 80 milioni.

Sisi tuna shida 80 milioni ukigawanya kwa Kamati 23 Bwana Spika inamaanisha kuwa kila Kamati inapata milioni tatu nukta tano.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mwanzo nasimama kuunga mkono hii hoja...

(*Applause*)

Sisi tumekuwa tunangoja uwepo wetu kutumia pesa hatuna njia nyengine ya kuuliza pesa zapatikana vipi ndani ya Nyumba hii, kwa hivyo hii itakuwa ni majukumu ya Bodi...

Kwa hivyo Bodi itoke ikatafute pesa; kuna wafadhili wengi ambao wanaweza kuleta pesa na kutoa ile idadi...

(*Applause*)

Tutafute *partners* wajua kuna *sponsors* na tuwe na *partners* na *associations* kina CMC kina nani, ziko nyingi sana zenye zinaweza kutia mkono wao zikatusaidia sisi ili kuweza kuliinua hili basi lenye laweze kusaidia wale watakao kuja siku za usoni.

Lakini la msingi ni kuwa iko na haja ya *Assembly* kuwa na basi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Duncan?

**Hon. Onyango:** Ahsante Mheshimiwa Spika, mimi naiunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika tumepitisha mswada huu inamaanisha kwamba vile vitu zote tumepitisha zitekelezwe na kwa jirani yangu ambaye ni ndugu yangu wa Miritini sijui zile shule na mahospitali amejenga anataka tusingitumie akitoka kwa mamlaka...

(*Applause*)

Mheshimiwa Spika kuna haja kubwa sisi kama *Assembly* tuwe na njia ya usafiri; kama vile wenzangu wamezungumza zile zitakazo patikana isiwe hoja sana sisi haja yetu kama Bunge ni ya kwamba tumepitisha Nyumba hii tuwe na basi ambayo inaweza kutoka *point A* hadi *Point B* ili kuweza kurahisisha shughuli za Nyumba hii. Ahsante sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Fadhili?

**Hon. Mwalimu:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama mbele ya Nyumba hii kupinga hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika ni juzi tu nimesikia Rais wa Jamhuri ya Kenya akisema kuwa hao wanakula nyama na wengine wanameza mate.



Mheshimiwa Spika hali ya wananchi wetu iko chini, serikali yetu ya Mombasa pamoja na Jumba letu hili kuna mambo mengi ambayo tunahitajika kuyafanya ambayo ni muhimu ambayo yanaleta natija kwa Wananchi wetu kuliko hili basi ambalo Waheshimiwa wenzangu wanalipigania kulipata.

Mheshimiwa Spika mimi nashangaa ikiwa Nyumba hili leo bado yavuja, sisi twafikiria kununua basi; tusiwache akili kubwa zikatawala akili ndogo, ama wengi wakatawala wale wachache, wacha sauti za sisi wachache zisikike...

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika kwa kusema kweli twajua umuhimu na mimi naheshimu sauti zilizozungumza kama sauti ya Kiongozi wa Walio Wengi anawakilisha serikali na anawakilisha Bodi ya Bunge la Kaunti.

Nimesikia Mwenyekiti wa Fedha Mheshimiwa Spika pia alivyozungumza; lau tutachukua, au aliyeleta hoja hii kusikia yalizongumzwa na Kiongozi wa Walio Wengi pamoja na Mwenyekiti wa Fedha, lau atachukua maono kama yale ili tuombe Bodi itafute wafadhili maana wafadhili wako.

Ni juzi Kiongozi wa Walio Wengi alieleta habari ndani ya Bunge hili kuwa (??) la safari hili linafanya mambo yake ndani ya Kaunti ya Mombasa, kwa nini tusichukue fursa hii tuwaombe nao watuchukulie sisi kama *Assembly* ya Kaunti hii badala ya kutumia pesa ambazo ziko katika bajeti ya *Assembly*.

Mheshimiwa Spika kama sasa hivi tunaona kuwa yale mambo ya maendeleo katika *Assembly* yamezuiwa, leo hii tena vipi tuseme twataka kufanya maendeleo...

*(Interruption)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Dan?

**Hon. Onyango:** Mheshimiwa anayezungumza anatuchanganya ya kwanza amesema anapinga ya pili anasema tuombe *Port* itunulie basi...

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Fadhili.

**Hon. Mwalimu:** Mheshimiwa mimi ninapinga tena nasema napinga pesa za Bunge la Kaunti zitumiwe kununua basi.

Mheshimiwa Spika mimi nasema tutafute wafadhili ama kama waheshimiwa wataweza kutoa ndani ya mifuko yao tufanye mchango ili tuweze kununua basi pasi na kutumia pesa za mwananchi.

Mheshimiwa Spika tunajua sasa hivi tunaenda au tunakaribia kuenda kufanya kura; kuna mengi ambayo yanahitaji sisi kufanya, kuna *Bills* nyingi hapa ambazo ziko, zingine bado zinataka kuenda kuhusisha Wananchi, kwa nini tusitoe pesa yetu kuenda kuhusisha wananchi watuongeze kama zile ili zirudi ndani ya Bunge hili na ziweze kupitishwa ndani ya Bunge hili na tuweze kuleta faida ndani katika Kaunti yetu...

Tuwache mambo yale tuende tukaweke pesa zetu kwa kunua basi Mheshimiwa Spika mimi nawaomba wenzangu tuungane pamoja tupinge hoji....

*(Applause and laughter)*

Nawaomba Mheshimiwa Spika sauti ya wachache iweze kusikika; na iwe ya mara kwanza sauti ya wachache imesikika ndani ya Bunge letu. Ahsante Mheshimiwa Spika.

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Mheshimiwa wa Mwakirunge.

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama hapa kuunga mkono...

*(Applause)*

Mheshimiwa Spika kwa ile haki na ule ukweli kufikia sasa nafikiri Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha yuko hapa ukiangalia zile pesa ambazo tumetumia kwa upande wa usafiri kupitia magari tungekuwa tumenunua basi mbili....

*(Applause)*

Najua hizo pesa ni nyingi na tungekuwa tumenunua basi mbili. Mheshimiwa Spika hili basi ambalo tunataka kununua....

*(Interruption)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Kibwana what is it?

**Hon. Kibwana Swaleh:** Hon. Speaker I just wonder the Hon. has gone to Nairobi, they use another means of transport and by the way there is transport allowance which is being budgeted.

So it doesn't mean that when we are being given an allowance to go to Lamu and we are given money it is a waste; there's transport allowances which is being budgeted so I think Hon. Speaker my colleague is misleading the House...

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika...

*(Interruption)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Amur Murfad.

**Hon. Amur:** Mr. Speaker buying the bus is not an issue but maintaining the bus is the issue...

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. of Mwakirunge can you continue.

**Hon. Mwinga:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika nafikiria Mheshimiwa Amur asimame aelezee kama ana *interest* kuhusiana na suala hili.

**Hon. Amur:** Mr. Speaker I declare that I have no interest.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Amur I have not given you permission to talk, yes continue Hon. Enock Mwinga.

**Hon. Mwinga:** Mheshimiwa Spika Kaunti hii kama vile nilivyosema ni Kaunti kubwa Kenya nzima.

Mheshimiwa Spika nisaidie kidogo hapa...

*(Interruption)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Fadhihi muache mwenzako azungumze wewe umezungumza na hakuna aliyekutatiza.

**Hon. Mwinga:** Mheshimiwa Spika mimi sisemi ni kubwa Kenya hii nasema ni kubwa...

*(Interruption)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Members let him talk, members! Members! Members the Speaker is standing everybody to sit.



Members if you want to talk just stand don't address the talker address me so Hon. Fadhili don't address the person who is talking if you want to speak communicate to me let's respect the Standing Orders but we don't talk freely as if this is not a Honorably place.

Thank you. Yes Hon. Hatimy.

**Hon. Mohamed Hatimy:** Mheshimiwa Spika nataka nimjibu Mheshimiwa mwenzangu kuwa Kaunti ya Mombasa ndio Kaunti ndogo kuliko Kaunti zote 47.

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Okay thank you Hon. for following the procedure, yes Hon. Paul Onje what is it?

**Hon. Onje:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika mimi nimesimama kidogo kumsaidia Mheshimiwa mwenzangu kwa hilo jambo la kusema Kaunti ya Mombasa ni kubwa angesema katika upande wa ukusanyaji wa mapato Kenya nzima inajua Kaunti ya Mombasa ni ya pili katika kuchangia pesa inayoenda serikali kuu.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank you Hon. Onje for following the Standing Order, continue Hon. Mwinga.

**Hon. Mwinga:** Mheshimiwa Spika nafikiria Kiswahili changu kidogo hakikueleweka...

*(Laughter)*

Lakini mimi ilikuwa namaanisha kuwa Kaunti yetu ni ya pili katika ukusanyaji ushuru Mheshimiwa Spika na ni ukweli.

Mheshimiwa Spika kama Kaunti yetu ni ya pili katika kukusanya mapato kwa nini tunashindwa kununua basi Mheshimiwa Spika hii ni kazi ndogo Mheshimiwa Spika hakuna haja kwenda kwa wafadhili Kaunti yetu ya Mombasa ina uwezo wa kununua basi Mheshimiwa Spika...

*(Interruption)*

**Hon. Mwalimu:** Mheshimiwa Spika mzungumzaji anasema kuwa kununua basi ni kazi ndogo lakini kununua basi kutahitaji kuliangalia kama mtoto mchanga.

Mheshimiwa Spika tutataka tuweke dereva, tuongeze mipango ya kuli *maintain* hilo basi...

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Mheshimiwa Fadhili you are contributing to the Motion. Yes Hon. Enock.

**Hon. Mwinga:** Mheshimiwa Spika Mheshimiwa ambaye ametoka kuongea nadhani anataka kupotesha hili Jumba.

Mheshimiwa Spika kuna magari ambayo yamenunuliwa ndani ya Mombasa Kaunti; hata wewe umenunuliwa gari na linakuwa *maintained* vizuri.

Mheshimiwa Spika akituambia ya kwamba hili basi halitakuwa *maintained* anapotosha hii Nyumba.

Kwa hivyo mimi nimesimama kuunga mkono nikasema kwamba basi linunuliwe ili Mheshimiwa Spika nipate kurahisisha kazi ndani ya Mombasa Kaunti. Ahsante.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank you very much, yes Hon. Paul Onje.

**Hon. Onje:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mimi nimesimama nikiunga mkono...

*(Applause)*

Na kitu kidogo ningependa nijue ni kwamba tungejua basi ambalo tunataka kununua ni la aina gani? Na iwapo tutanunua basi ambalo linabeba watu 28 basi Mheshimiwa Spika hilo moja basi litakuwa halitoshi kwa sababu gani saa zengine tunatoka na wafanyi kazi wetu na sisi wenyewe tuko 44 pamoja na *Nominated* na wale wafanyi kazi tuko na *Sergeant at Arms*.

Kwa hiyo tukinunua Mheshimiwa Spika gari moja halitatosha ni heri tujue ni aina gani na kama ni gari mbili sawa na itasaidia mambo ya *site visit* lataka tuliunge mkono sana. Ahsante sana.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Yes Hon. Zainab Said Ali.

**Hon.(Ms.) Zainab Said:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono...

*(Applause)*

Naiunga mkono kwa sababu Mwenyekiti wa Fedha amesema pesa hakuna lakini tutafute wafadhili ama hawa wafadhili ndio hamuwataki? Hili basi litakuwa ni la watu wa Kaunti...

*(Applause)*

Kwa hivyo hilo gari tufanye bidii tupate wafadhili ili tuepoke ufujaji wa pesa, kwa hivyo wafadhili wakitusaidia basi moja na *Nissan* moja yatoshia na tutapata hizo gari kutoka kwa wafadhili. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Members if you agree all the three Members that you are up you have already contributed. Yes what is it Hon. Onje, but you have already contributed.

**Hon. Onje:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi, mimi nataka kumuomba Mheshimiwa mwenzangu Fadhili kwa sababu gani akisikia Mheshimiwa Zainab Said anasema tutatafuta wafadhili watununulie basi...

*(Laughter)*

Basi Mheshimiwa Fadhili anafikiria ni Fadhili...

*(Laughter)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Hatimy.

**Hon. Mohamed Hatimy:** Mr. Speaker I rise under Standing 51; I request the mover of this Motion under Standing Order 48 to withdraw the Motion under Standing Order 48.

**Hon. Mwalimu:** Is the mover willing Mr. Speaker?

**Hon. Mohamed Hatimy:** I am requesting the mover to withdraw under Standing Order 48 and remember I said I rise under Standing order 51 to amend this Motion so as to come back again to the House. Thank you Mr. Speaker.

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): The mover of the Motion are you in agreement with the request of Hon. Hatimy?

**Hon.(Ms.) Zainab Kithinzi:** Yes I do agree.

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Thank you, the Motion has been withdrawn...

*(Applause)*

So it will come back with amendments...

*(Applause)*

**Hon. Mwalimu:** Bwana Spika mimi nataka kufahamisha Jumba hili leo sauti ya wanyonge imesikika...

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Hon. Hatimy what is it?

**Hon. Mohamed Hatimy:** Sijui kama hapa kuna wanyonge ama nini? Nataka kujua wanyonge ni kina nani?

*(Applause)*

**The Deputy Speaker** (Hon. Mswabah Rashid): Okay Members the Motion has been withdrawn and it will come back after being amended. Clerk?

#### **ADJOURNMENT**

Members there being no other business this House stands adjourned until today in the afternoon.

The House rose at 10:07am.